

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA**

Simu Nambari: 2152532/3  
Baruapepe: [cg@dcea.go.tz](mailto:cg@dcea.go.tz)  
Tovuti: [www.dcea.go.tz](http://www.dcea.go.tz)  
Nukushi: 2152820



8Barabara ya kivukoni,  
S.L.P. 80327,  
Dar es Salaam.

**TAARIFA KWA UMMA**

**MAHAKAMA YAMUHUKUMU KWENDA JELA MIAKA 30 MSHTAKIWA WA DAWA ZA KULEVYA**

Dar es Salaam, 08 Mei 2020:

Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, imemuhukumu kutumikia kifungo cha miaka thelathini (30) jela mshtakiwa **Islem Shebe Islem (50)** kwa kosa la kusafirisha dawa za kulevya aina ya heroin zenye uzito wa gramu 306.32.

Hukumu hiyo imetolewa leo mbele ya Mhe. Jaji E. B. Luvanda baada ya ushahidi uliotolewa mahakamani hapo kuthibitisha pasipo shaka yoyote kwamba mshtakiwa ni mfanyabiashara wa dawa za kulevya.

Islem alikamatwa na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya tarehe 20/07/2018 eneo la Magomeni Usalama, wilaya ya Kinondoni jijini Dar es Salaam akiwa na dawa hizo na kufunguliwa kesi ya uhujumu uchumi namba 11 ya mwaka 2019.

Mshtakiwa ametiwa hatiani kwa kukiuka Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Namba 5 ya mwaka 2015 kama ilivyorekebishwa na Sheria Namba 15 ya mwaka 2017.

Imetolewa na,

A handwritten signature in blue ink, appearing to read 'Florence Khambi'.

Florence Khambi

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano

**Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya**